# UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Simu: +(257) 22 248636
Nukushi : +(257) 22 248637
Barua pepe: tanzanrep@usan-bu.net

Kinindo
Avenue Du Large,
Nyumba namba. 51,
S.L.P 855,
BUJUMBURA,
**BURUNDI.**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb.Na. CHAB 357/448/01/20**

**02 Aprili, 2020**

**Watanzania wote nchini Burundi**

KUH: **TAARIFA YA WIZARA YA AFYA YA BURUNDI KWA UMMA KUHUSIANA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA SERIKALI KWA AJILI YA KUJIKINGA NA KUPAMBANA NA UGONJWA WA HOMA YA MAPAFU (COVID-19)**

Kufuatia kuwepo kwa ugonjwa wa homa ya mapafu (COVID-19) unaosababishwa na Kirusi cha Corona, Wizara ya Afya na Mapambano dhidi ya Ukimwi ya Jamhuri ya Burundi imetoa taarifa kwa umma na kwa Jumuiya ya Kimataifa juu ya hali ya ugonjwa huo nchini na kuelekeza ifuatavyo:-

1. Hali ya wagonjwa wawili waliogundulika kuwa na ugonjwa wa COVID-19 nchini hapo tarehe 31 Machi, 2020 ambao wamelazwa katika kituo cha matibabu cha hospitali ya Prince Louis Rwagasore, inaendelea vizuri;
2. Serikali inapenda kutoa taarifa kwamba imeishachukua hatua ya kuwatenganisha wagonjwa wa COVID-19 waliopo katika hospitali ya Prince Louis Rwagasore na wagonjwa wengine wanaopata matibatu hapo. Hivyo, watumiaji wa hospitali hiyo waendelee kuitumia bila woga wa kupata maambukizi ya virusi vya Corona.
3. Kazi ya kuwatambua na kuwaweka karantini watu waliokutana na wagonjwa hao wawili inaendelea ili wote wapimwe kuona kama na wao wameambukizwa virusi vya ugonjwa;
4. Mtu yoyote aliyepimwa na kugundulika ameambukizwa vizuri vya Corona haina maana atafariki. Hivyo Wizara ya Afya inawataka wananchi waendelee kuwa watulivu, wananchi waendelee na shughuli zao kama kawaida na waendelee kuzingatia na kuheshimu taratibu za kujikinga na ugonjwa huo zilizotangazwa na Wizara kama ifuatavyo:-

i) Kunawa mikono kwa maji safi na sabuni au na maji yaliyotiwa chlorine;

ii) Epuka kusalimiana kwa kupeana mikono au kwa kubusiana;

iii) Kohoa au piga chafya ukiwa umeziba mdomo wako na kiwiko au tumia tishu na kuiweka kwenye chombo cha kuwekea uchafu na kisha nawa mikono yako.

5. Wizara inawakumbusha tena wananchi kutokuamini taarifa za uvumi zinazotolewa na mitandao ya jamii au vyombo vingine vya mawasiliano.
6. Wizara inamtaka mtu yeyote ambaye amekutana na mtu aliyeambukizwa na vizuri vya Corona ambaye bado hajaonesha dalili za kuugua ugonjwa wa COVID-19 kujiweka karantini yeye mwenyewe nyumbani kwake. Na ikiwa dalili zitaonekana, basi ni lazima afike katika kituo cha afya cha karibu haraka iwezekanavyo au apige simu namba 117.
7. Wizara ya Afya inatoa tena wito kwa wananchi kwamba uvaaji wa "Mask" ni kwa ajili ya watu walioathirika na ugonjwa wa COVID-19 na watoa huduma ya afya na siyo kila mtu.
8. Mwisho, Wizara inatoa shukrani na pongezi kwa watoa huduma wote wa afya ambao wako mstari wa mbele, mchana na usiku, katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu (COVID-19) unaosababishwa na kirusi cha Corona.

Ubalozi unawaombea vyote kuwa salama na kuweni makini na kujiepusha na misongamano ya aina yoyote na kufuata masharti yote ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo hatari.

Mwenyezi Mungu atubariki na kutulinda sote.

Dkt. Edmund J. Kitokezi

Kny: **BALOZI**